TAARIFA ZA AWALI ZA TOLEO NA MAELEKEZO YA JUMLA

KIAMBATANISHI – I

SEHEMU - I: TAARIFA ZA TOLEO:

1. MUHTASARI WA MFUKO WA WEKEZA MAISHA:

- **Madhumuni:** ni mpango wa wazi wa muda mrefu unaokusudia kukuza mtaji na kwa wakati huo huo ukitoa kinga ya Bima ya Maisha, Bima ya Ajali/ Ulemavu wa Kudumu na Gharama za Mazishi.
- **Chaguo la Mpango wa Uwekezaji:** Mfuko unatoa fursa mbili za uwekezaji – (a) Mpango wa Uwekezaji kwa Awamu na (b) Uwekezaji wa Mkupuo.
- **Nani anaruhusiwa kuwekeza na umri wa kujiunga:** Mfuko uko wazi kwa Mtanzania aliye ndani na nje ya nchi mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 55.
- **Ukomo wa Uwekezaji:** Uwanachama wa mwekezaji katika mfuko huu utakoma baada ya miaka 10.
- **Ukwasi:** Uuzaji wa sehemu ya uwekezaji (baadhi ya vipande) katika mfuko unaruhusiwa baada ya miaka 5
- **Thamani ya Mwanzo ya Kipande:** Thamani ya mwanzo ya kipande (face value) ni Shs.100/=
- **Bei ya Kipande:** Bei ya kipande ni Sh. 100/- wakati wa mauzo ya mwanzo, yaani kuanzia tarehe 16 Mei 2007 hadi 31 Julai 2007 na baada ya hapo kipande kitauzwa kulingana na thamani halisi ya soko (Net Asset Value).
- **Kiwango cha Kuwekeza: (a)** Kiwango cha chini :- ni Shs. Milioni 1 na **(b)** hakuna kiwango cha juu cha kuwekeza (Lakini mafao ya Bima ya maisha yatatolewa mpaka kufikia kiwango cha Shs. Milioni 25 tu)
- **Mafao ya Bima ya Maisha (Kifo au ulemavu wa kudumu): (a)** Mpango wa Kuwekeza kwa Awamu: Kinga ya Bima ya maisha ni sawa na kiasi kisicholipwa na mwekezaji kwa muda uliosalia katika mpango wake wa uwekezaji (Muhimu: kiwango cha juu kulipwa ni Shs. Milioni 25 **(b)** Mpango wa kuwekeza kwa Mkupuo: Kinga ya Bima ya maisha itakuwa sawa na kiwango alichochagua mwekezaji. (Muhimu: kiwango cha juu kulipwa ni Shs. Milioni 25)
- **Mafao ya Bima ya Ajali:** Mwekezaji atalipwa asilimia 20 ya kiwango kilichokusudiwa katika mpango wa uwekezaji, hata hivyo kiwango cha juu ni shs. Milioni 5 tu.
- **Mafao ya Gharama za Mazishi:** Kila mwekezaji atalipwa Shs 500,000/- kwa ajili ya mazishi endapo atafariki bila kujali kiwango alichowekeza***. Mafao haya yatalipwa kwa wawekezaji watakaoingia wakati wa mauzo ya mwanzo tu.***
- **Mkono wa Kheri (Loyalty Bonus):** Mfuko utatoa mkono wa kheri kwa mwekezaji ambaye atakamilisha miaka kumi ya mpango wake wa uwekezaji au kama atafariki ndani ya mwaka wa mwisho wa mpango wake wa uwekezaji.

2. KIASI CHA KUWEKEZA

Maombi ya mauzo ya mwanzo yatatokana na kiasi kilichochaguliwa kuwekezwa (chosen contribution amount) na pia aina ya malipo iliyochaguliwa (chosen contribution option).

(A) MPANGO WA KUWEKA AKIBA KWA AWAMU

Kutokana na kiwango kilichokusudiwa kuwekezwa mwekezaji anaweza kuwekeza kwa awamu, Mpango wa kuwekeza kwa awamu unaweza kufanyika kila mwezi (monthly), kila baada ya kipindi cha miezi sita (six monthly), au kila mwaka (annually) kama inavyoainishwa hapa chini:

(A.1) AINA ZA MALIPO:

Jedwali la Michango kwa Awamu: Mfano

Kiwango cha Mchango kilicho kusudiwa (Shs.)	Kiwango cha Mchango kila mwezi	Kiwango cha Mchango kila baada ya miezi sita	Kiwango cha Mchango kila mwaka
Millioni 1	8,340	50,000	100,000
Millioni 2	16,670	100,000	200,000
Millioni 3	25,000	150,000	300,000
n.k			
Millioni 25	208,340	1,250,000	2,500,000
Millioni100	833,340	5,000,000	10,000,000
Millioni 500	4,166,670	25,000,000	50,000,000

(A.2) JINSI YA KULIPA:

Malipo yanaweza kulipwa kila mwezi, kila baada ya miezi sita, au kila mwaka kwa kupitia njia zifuatazo:

	NAMNA YA MALIPO
I	Mwekezaji anaweza kulipa moja kwa moja mwenyewe (Own arrangement).
II	Mwekezaji anaweza kulipa moja kwa moja kwa kupitia benki yake (Bankers instruction)
III	Mwekezaji anaweza kulipiwa na mwajiri wake kutoka kwenye mshahara wake. (Salary Saving Scheme)

(A.3) KWA MALIPO YA KILA MWEZI – JINSI YA KULIPA MALIPO YA MIEZI INAYOFUATA (MWEZI WA 2,3,4, NA WA 5) KWA WAWEKEZAJI WALIONUNUA VIPANDE WAKATI WA MAUZO YA MWANZO:

- Kwa mwekezaji atakayechagua mpango wa kuwekeza kwa awamu atatakiwa kulipa malipo ya mwanzo wakati wa kujiunga na mfuko (Katika kipindi cha mauzo ya mwanzo 16 Mei mpaka 31 Julai 2007)
- Kwa malipo ya awamu ya 2, 3, 4 na 5 mwekezaji atatakiwa kulipa michango yake tarehe 1 Desemba 2007, katika kipindi hicho meneja atakuwa amewafahamisha wamiliki wa vipande akaunti zao za uwekezaji katika mfuko wa Wekeza Maisha.
- Na baada ya hapo michango kwa ajili ya awamu zinazofuata itawasilishwa katika kila siku ya kwanza ya kazi katika kila mwezi.
- Na kila mchango utalipwa ndani ya siku kumi za kazi tangu mchango ulipostahili kulipwa.

- Kama jedwali lifuatalo linavyoeleza:

Awamu (Installment Number)	**Siku ya Mchango**	**Maelezo**
1	Mauzo ya Mwanzo	
2	1 Desemba 2007	Kwa wale ambao watakaojiunga na mfuko katika mauzo ya mwanzo, Michango kwa ajili ya awamu ya 2,3,4,na 5 yatalipwa kwa pamoja.
3		
4		
5		
6	2 Januari 2008	Michango italipwa ndani ya siku kumi za kazi
7	1 Februari 2008	
n.k		

Muhimu: Pamoja na kwamba mwekezaji anaweza kulipa michango yake ndani ya siku kumi za kazi, thamani ya kipande itakayotumika itategemea siku ambayo mwekezaji atakuwa amelipa, hivyo basi ,kuchelewa kulipa hakutamuongezea faida yoyote mwekezaji.

(B) ULIPAJI WA MICHANGO KWA MKUPUO

Kiwango cha mchango kilichokusudiwa na mwekezaji kitawekezwa kwa mkupuo wakati wa kuingia uanachama wa mfuko:

(B.1) Jedwali la michango kwa mpango wa mkupuo (Mfano):-

Kiwango kilicho kusudiwa kuwekezwa(Tzs)	**Kiwango cha Malipo kwa Mkupuo (Tzs)**	**Kiwango kilicho kusudiwa kuwekezwa(Tzs**	**Kiwango cha Malipo kwa Mkupuo (Tzs)**
1 Milioni	1 Milioni	20 Milioni	20 Milioni
2 Milioni	2 Milioni	25 Milioni	25 Milioni
3 Milioni	3 Milioni	50 Milioni	50 Milioni
4 Milioni	4 Milioni	100 Milioni	100 Milioni
5 Milioni	5 Milioni	500 Milioni	500 Milioni
and so on	….	….	….
10 Milioni	10 Milioni	1 Bilioni	1 Bilioni

3. BIMA YA MAISHA WAKATI WA KIFO NA ULEMAVU WA KUDUMU

(a) **MPANGO WA KUWEKA AKIBA KWA AWAMU –** Mafao ya Bima ya Maisha katika Mpango wa malipo kwa awamu yatapatikana kwa kutumia Michango ambayo haijalipwa na muda wa kulipa haujafika(***unpaid but not due amount)***. Lakini ukomo wa mafao haya ni shillingi Millioni 25 tu. .

Mfano (1) Michango ambayo haijalipwa na muda wa kulipa haujafika ':

- Fikiria kiasi kilichochaguliwa kuwekeza cha shs milioni 10
- Kiasi cha kuchangia kwa mwaka shs 1 Milioni (1/10 ya 10 Milioni

Tukio la Kifo	**Michango iliyolipwa**	**Michango ambayo haijalipwa na muda wa kulipwa haujafika**
Ndani ya mwaka wa kwanza (0 – 1)	Milioni 1	Hakuna Mafao ***(Hakuna mafao ya kifo au ulemavu yatakayotolewa kwa mwaka wa kwanza wa uanachama isipokuwa kwa kifo kitakachotokea kwa ajali tu ambayo mstahili atalipwa Shs milioni 9)***
Mwaka wa pili	Milioni 2	Milioni 8
Mwaka wa tatu	Milioni 3	Milioni 7
Mwaka wa nne	Milioni 4	Milioni 6
Mwaka wa tano	Milioni 5	Milioni 5
……..		
Mwaka wa tisa	Milioni 9	Milioni 1
Mwaka wa kumi	Milioni 10	Hakuna Mafao **(Hakuna mafao ya kifo /ulemavu yatakayotolewa mwaka wa 10 wa uwekezaji ingawa mwekezaji ana haki ya kulipwa mkono wa Pongezi*)***

<u>Mfano (2)</u> Michango ambayo haijalipwa na muda wa kulipa haujafika <u>:</u>

- Fikiria kiasi kilichochaguliwa kuwekeza Shs Milioni 25
- Kiasi cha kuchangia kwa mwaka Shs Milioni 2.5

Tukio la Kifo	**Michango iliyolipwa**	**Michango ambayo haijalipwa na muda wa kulipwa haujafika**
Ndani ya mwaka wa kwanza (0 – 1)	2.5 Million	Hakuna Mafao ***(Hakuna mafao ya kifo au ulemavu yatakayotolewa kwa mwaka wa kwanza wa uanachama isipokuwa kwa kifo kitakachotokea kwa ajali ambayo tu ambayo mstahili atalipwa Milioni 25)***
Mwaka wa pili	5 Milioni	20 Milioni
Mwaka wa tatu	7.5 Milioni	17.5 Milioni
Mwaka wa nne	10 Milioni	15 Milioni
Mwaka wa tano	12.5 Milioni	12.5 Milioni
……..		
Mwaka wa tisa	22.5 Milioni	2.5 Milioni
Mwaka wa kumi	25 Milioni	**Hakuna mafao ya kifo /ulemavu yatakayotolewa mwaka wa 10 wa uwekezaji ingawa mwekezaji ana haki ya kulipwa mkono wa Pongezi*)***

Muhimu: Gharama za bima zitalipwa kama asilimia ya kiwango cha uwekezaji kitakachochaguliwa na mwekezaji kila mwaka isipokuwa kiwango hicho cha uwekezaji kisizidi Shs. Millioni 25 – kwa maana ya kwamba mwekezaji atayewekeza zaidi ya shs. Millioni 25, gharama za bima zitalipwa kwa ajili ya Shs. Millioni 25 tu na siyo zaidi ya hapo.
.

(b)MPANGO WA KUWEKEZA KWA MKUPUO – Bima ya maisha itatolewa sawa na kiasi cha kuwekeza kilichochaguliwa (lakini haitazidi kiwango cha juu cha shs milioni 25):

Mfano (1): Fikiria kiasi kilichochaguliwa kuwekeza = Shs. Milioni 10

Tukio la Kifo	Kiasi kilichochaguliwa kuwekezwa (Tzs)	Kiasi kitakachowekezwa kwa bima ya maisha (Tzs)
Ndani ya mwaka wa kwanza (0 – 1)	Milioni 10	Hakuna Mafao ***(Hakuna mafao ya kifo au ulemavu yatakayotolewa kwa mwaka wa kwanza wa uanachama isipokuwa kwa kifo kitakachotokea kwa ajali ambayo tu ambayo mstahili atalipwa Milioni 10)***
Mwaka wa pili		Milioni 10
Mwaka wa tatu		Milioni 10
Mwaka wa nne		Milioni 10
Mwaka wa tano		Milioni 10
…….		
Mwaka wa tisa		Milioni 10
Mwaka wa kumi		Milioni 10

Mfano (2): Fikiria kiasi kilichochaguliwa kuwekezwa = Shs Milioni 25

Muhimu: Gharama za bima zitalipwa kama asilimia ya kiwango cha uwekezaji kitakachochaguliwa na mwekezaji kila mwaka isipokuwa kiwango hicho cha uwekezaji kisizidi Shs. Millioni 25 – kwa maana ya kwamba mwekezaji atayewekeza zaidi ya shs. Millioni 25, gharama za bima zitalipwa kwa ajili ya Shs. Millioni 25 tu na siyo zaidi ya hapo.
.

Tukio la Kifo	Kiasi kilichochaguliwa kuwekezwa (Tzs)	Kiasi kitakachowekezwa kwa bima ya maisha (Tzs)
Ndani ya mwaka wa kwanza (0 – 1)	Milioni 50	Hakuna Mafao ***(Hakuna mafao ya kifo au ulemavu yatakayotolewa kwa mwaka wa kwanza wa uanachama isipokuwa kwa kifo kitakachotokea kwa ajali ambayo tu ambayo mstahili atalipwa Milioni 25)***
Mwaka wa pili		Milioni 25 (Kiwango cha juu)
Mwaka wa tatu		Milioni 25 (Kiwango cha juu)
Mwaka wa nne		Milioni 25 (Kiwango cha juu)
Mwaka wa tano		Milioni 25 (Kiwango cha juu)
…….		Milioni 25 (Kiwango cha juu)
Mwaka wa tisa		Milioni 25 (Kiwango cha juu)
Mwaka wa kumi		Milioni 25 (Kiwango cha juu)

4. STAHILI YA MAFAO YA BIMA

SN	TUKIO	---MAFAO YA BIMA----		
		MAISHA	**AJALI**	**MAZISHI**
1.	Kifo	ndio	ndio (Kama kifo kimetokea kwa ajali)	Ndio
2.	Ulemavu wa kudumu kutokana na ugonjwa au ajali	ndio	hapana (*)	hapana
3.	Kupoteza kiungo / ufahamu inayotokana na ajali	hapana	ndio	hapana
Mwekezaji atanufaika na mafao ya bima ya maisha ambayo yana thamani kubwa kuliko mafao ya ajali hivyo hakutakuwa na malipo ya mafao ya ajali yatakayosababisha ulemavu wa kudumu.				

5.MKONO WA PONGEZI

Mfuko unao utaratibu wa kulipa Mkono wa Pongezi wakati wa mwisho wa uanachama au kifo wakati wa mwaka wa mwisho wa uanachama kwa kuzingatia kwamba malipo yote yalilipwa kwa wakati na hakuna mauzo ya baadhi ya vipande yaliyofanywa na mwekezaji.
Kiwango: asilimia 5 italipwa kwa mpango wa uwekezeji wa malipo kwa awamu na asilimia 7 italipwa kwa mpango wa uwekezaji kwa mkupuo. Mkono wa Pongezi utapatikana kwa kuanzisha akaunti maalum ambapo sehemu ya mapato ya Mfuko yatadundulizwa kila siku, ambapo itakuwa ni sehemu ya gharama kwa Mfuko

6. MAFAO YAPATIKANAYO WAKATI WA KIFO

Iwapo kifo cha ghafla kimetokea kwa mmiliki wa vipande wakati bado yuko kwenye mfuko, mrithi / mmiliki halali kisheria anayo haki kupata mafao yafuatayo:

(a) Mfuko utalipa vipande vilivyoachwa na marehemu kwa thamani ya vipande kwa wakati uliopo.

(b) Mtoa bima atalipa stahili ya kiasi kinachotakiwa kwa bima ya maisha kama ilivyoainishwa katika aina za uwekezaji (regular & single contribution)*;*

(c) Mtoa bima atalipa stahili ya kiasi kinachotakiwa iwapo mwekezaji atapoteza maisha kwa ajali iliyotokea Tanzania.

(d) Mtoa bima atalipa gharama za mazishi kwa mmiliki wa vipande aliyewekeza wakati wa mauzo ya mwanzo.

(e) Mfuko utalipa mkono wa kwaheri ikiwa tu mwekezaji amepoteza maisha yake mwaka wa mwisho wa uanachama .

7. KUPEVUKA KWA MFUKO (UKOMO):

Yafuatayo yatalipwa baada ya mfuko kupevuka:

(a) Vipande vitalipwa kwa thamani ya bei ya kipande kwa wakati huo bila gharama yoyote .

(b) Stahili ya kiasi cha mkono wa kwaheri kitalipwa kwa mwekezaji isipokuwa kwa wale waliouza baadhi ya vipande wakati wa uanachama.

TAARIFA AWALI ZA TOLEO NA MAELEKEZO YA JUMLA

Muhimu: (a) Mwekezaji atakayejiunga na mfuko wakati wa mauzo ya mwanzo, kupevuka kwa vipande vyake baada ya miaka 10 kuanzia siku ya mwisho ya mauzo ya awali (31 julai 2007) (b) Mauzo ya mwekezaji atakayewekeza baada ya mauzo ya awali yatapevuka baada ya miaka 10 kuanzia siku aliyowekeza kama itakavyoainishwa kwenye

8. GHARAMA YA BIMA

(a) Gharama za bima zitalipwa na mwekezaji kwenye Kampuni ya Bima kupitia kwa meneja ili kupata kinga ya bima kama vile Bima ya maisha, Bima ya Ajali na Bima ya Mazishi kutokana na kanuni za bima.

(b) **Dhamana ya Uwekezaji Tanzania itagharamia gharama za bima kwa mwaka wa kwanza kwa wale wawekezaji watakaojiunga wakati wa mauzo ya awali. Na hivyo basi wawekezaji hawatalipa gharama za bima kwa mwaka wa kwanza na pesa zote zitanunulia vipande.**

(c) Gharama za bima zitalipwa kama asilimia ya kiwango cha uwekezaji kitakachochaguliwa na mwekezaji kila mwaka isipokuwa kiwango hicho cha uwekezaji kisizidi Shs. Millioni 25 – kwa maana ya kwamba mwekezaji atayewekeza zaidi ya shs. Millioni 25, gharama za bima zitalipwa kwa ajili ya Shs. Millioni 25 tu na siyo zaidi ya hapo.

(d) Kwa sasa gharama hizi kwa mwaka ni kama ifuatavyo:

Na.	MPANGO WA UWEKEZAJI	Asilimia ya gharama za Bima kwa mwaka
1.	Malipo ya Awamu	**0.479 y**a kiasi cha Uwekezaji isipokuwa zaidi ya Shs. Millioni 25.
2.	Malipo ya mara moja	**0.870** ya kiasi uwekezaji isipokuwa zaidi ya Shs. millioni 25.

(e) Kiasi kinachobaki (baada ya gharama za bima) kitawekezwa ili kupata vipande kwa kutumia thamani ya vipande inayotumika kwa siku hiyo.

(f) Katika mpango wa malipo kwa awamu, kiasi cha malipo ya bima kitalipwa kwenye Kampuni ya Bima kutoka kwenye uwekezaji wako wa awamu.

(g) Katika Mpango wa Malipo kwa mkupuo, gharama za bima zinalipwa kwenye Kampuni ya bima kutoka katika uwekezaji wako wa mkupuo .Na baada ya hapo malipo ya gharama ya bima yatalipwa baada ya kupunguza vipande kwa thamani ya kipande ya siku hiyo.

(h) Kiwango cha gharama za bima kinaweza kubadilika kulingana na mabadiliko ya bei (tafadhali soma Kanuni za bima)

Jedwali la Gharama za bima kwa mwaka. **Mfano**

Na.	Kiasi cha Uwekezaji (Tzs)	-Mpango wa malipo kwa awamu-		-Mpango wa Malipo kwa Mkupuo-	
		Kiwango(asilimia)	Kiasi kwa mwaka. (Tzs)	Kiwango(asilimia)	Kiasi kwa mwaka. (Tzs)
1.	Millioni 1	**0.479** ya kiasi cha uwekezaji isipokuwa kiasi hicho kisizidi shilingi Milioni 25	4,790	**0.870** ya kiasi cha uwekezaji isipokuwa kiasi hicho kisizidi shilingi Milioni 25	8,700
2.	Millioni 2		9,580		17,400
3.	Millioni 3		14,370		26,100
4	Millioni 4		19,160		34,800
5.	Millioni 5		23,950		43,500
..					
10.	Millioni 10		47,900		87,000
..					
20.	Millioni 20		95,800		174,000
..					
25.	Millioni 25		119,750		217,500
..					
30.	(*)Millioni 30		119,750		217,500
50.	(*)Million 50		119,750		217,500
..					
100.	(*)Million 100		119,750		217,500
…					
200.	(*)Million 200		119,750		217,500

(*)Kwa wale watakaowekeza zaidi ya millioni 25 basi gharama za bima zitakatwa kwa kiasi cha shs. Milioni 25 tu.

9. KUNUNUA VIPANDE ZAIDI YA MARA MOJA KATIKA MFUKO WA WEKEZA MAISHA.

(a) Mwekezaji anaweza kujiunga na mfuko zaidi ya mara moja ili mradi tu asizidi miaka iliyoainishwa.

(b) Mwekezaji atayependa kununua vipande zaidi ya mara moja atafanya hivyo iwapo tu atatumia nambari akaunti hiyo hiyo ya uwekezaji na atachagua mwakilishi huyohuyo wa mwanzo.

Muhimu: Iwapo mwekezaji hatafanya kama inavyoelekezwa hapo juu, kuna hatari za kupoteza faida mbalimbali zitokanazo na uwekezaji.

(c) Kama utawekeza zaidi ya mara moja , Mahesabu ya faida za bima yatafanywa kulingana na kiasi cha uwekezaji kilichochaguliwa na mwisho wa kulipwa faida za bima ya shs. Milioni 25 kwa bima ya maisha shs.milioni 5 kwa bima ya Ajali na shs. 500,000/- kama gharama za mazishi.

10. KUSITISHWA KWA BIMA (TERMINATION)

Bima itakwisha iwapo kutatokea mojawapo ya mambo yafuatayo:

(a) Kifo au kilema cha kudumu kwa mmiliki wa vipande- Mwekezaji atalipwa mafao ya bima ya maisha au ya ulemavu.

(b) Baada ya muda wa mpango wa mwanachama kuiva/ kupevuka (Maturity of the plan)- mwekezaji atalipwa mafao (Maturity benefits)

(c) Kama uanachama umesitishwa kutokana na kutolipa mchango- mwekezaji atalipwa thamani ya vipande vyake hadi kufikia siku aliyolipia mchango.(Isipokuwa pale tu mwekezaji atakapoamua kufufua mpango wake wa uwekezaji)

(d) Kama mwakezaji atakoma kuwa mwanachama.

Muhimu:

1. Wakati wa tukio la kifo/kilema cha kudumu mwekezaji atalipwa mafao ya bima ya maisha/ulemavu
2. Wakati wa kupevuka kwa mfuko mwekezaji atalipwa mafao(maturity benefits)
3. Kama uanachama utasitishwa kutokana na kutolipa michango mwekezaji atalipwa stahili ya vipande kufuatana na bei ya kipande kwa wakati huo baada ya kulipa gharama za huduma ambazo hazitazidi asilimia 2 ya bei ya kipande.

SEHEMU – II: MAELEKEZO YA JUMLA

1. Tafadhali rejea taarifa zilizotolewa kwenye Waraka wa Toleo. Mwombaji awasiliane (kama atahitaji) na wataalamu wa masuala ya fedha, bima, uwekezaji au mwanasheria atakapojaza fomu ya maombi ya kujiunga.

2. Mfuko utakuwa wazi kwa mauzo ya mwanzo kuanzia 16 Mei 2007.

3. Jaza taarifa zote kwa kutumia herufi kubwa. Tumia kisanduku kimoja kwa kila herufi. Maombi yafanywe kwenye fomu halisi tu nakala, faksi au durufu zozote hazitapokelewa.

4. Wakati wa mauzo ya mwanzo vipande vitauzwa katika ofisi za mawakala zifuatazo:

   - **Wakala wa Kukusanya fedha**: Benki ya CRDB, Benki ya EXIM, Benki ya Posta,Shirika la Posta na wakala wa soko la hisa la Dar Es Salaam – Tanzania Securities, Solomon Securities, Orbit Insurance , Vertex International Ltd & Core Securities Limited.

   - **Wakala wa Mauzo:** Wakala wa Bima – Alexander Forbes, Busara Insurance, Astra Insurance, Orbit Insurance,mega Insurance, Citizen Insurance,Millenium Insurance,Intertrade Express , F&P Insurance , British Tanzania Insurance, Corporate Insurance & Rova Services.

5. Kumbuka, usitoe pesa kwa mtu yeyote asiye wakala aliyeteuliwa na baada ya kukabidhi pesa na fomu ya maombi hakikisha unapata risiti kutoka kwa wakala aliyeteuliwa. **Muhimu: Wakala wa Bima wanaruhusiwa kufanya mauzo ya vipande isipokuwa hawaruhusiwi kupokea fedha taslimu/hundi. Wawekezaji wa vipande wanaombwa kulipia fedha hizo katika tawi lolote la benki ya CRDB iliyo karibu.**

6. Kila fomu ya maombi iambatanishwe na pesa taslimu au hundi itakayolipwa kwenye akaunti ya Wekeza Maisha. Namba ya maombi iandikwe nyuma ya hundi itakayotumika kufanya manunuzi ya vipande.

7. Fomu itakuwa imekamilika pale tu kiasi cha kuwekeza kitakapokuwa kimetajwa pamoja na jinsi ya kuwekeza (Kwa mkupuo au kwa awamu) na njia za malipo (kila mwezi, kila miezi 6 au kwa mwaka) wakati wa kuwekeza.

8. Mfuko huu unahusisha masuala ya Bima hivyo mwekezaji analazimika kujaza taarifa ya tarehe ya kuzaliwa.

9. Fomu ya maombi ikishajazwa iwasilishwe pamoja na pesa taslimu kwa wakala wa kukusanya fedha waliotajwa hapo juu.

10. Mabadiliko yoyote katika fomu ya maombi yathibitishwe kwa sahihi kamili ya mwombaji.

11. Maombi yote yakishawakilishwa hayatarudishwa kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa Toleo.

12. Baada ya mauzo ya mwanzo wamiliki halali wa vipande watatumiwa Taarifa ya Akaunti kuonyesha idadi ya vipande wanavyomiliki.

13. Mauzo yanayofuata: Mfuko utakuwa wazi kwa mauzo ya vipande baada ya miezi sita ya mauzo ya mwanzo (1 Februari 2008).

14. Mauzo ya baadhi ya vipande: Mauzo ya baadhi ya vipande (sehemu ya uwekezaji) yataruhusiwa baada ya miaka mitano ya mauzo ya mwanzo.(1 Agosti 2012)

15. Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ina haki ya kukataa maombi yoyote. Maamuzi yoyote ya Dhamana ya Uwekezaji ya stahili au kutostahili kumiliki vipande ni ya mwisho baada ya kupata uamuzi wa Waziri.

16. Kumbuka ni muhimu kuweka sahihi kwenye fomu yako ya maombi kwani maombi yasiyo na sahihi yatakataliwa na Meneja. Kuweka sahihi yako kwenye fomu ya maombi inathibitisha pia afya njema.

FAIDA ZA ZIADA ZINAZOPATIKANA WAKATI WA MAUZO YA MWANZO

- Gharama za bima za mwaka wa kwanza zitalipwa na Dhamana ya Uwekezaji Tanzania hivyo pesa yote itatumika kununulia vipande.
- Iwapo mwekezaji atafariki dunia gharama za mazishi kwa mwekezaji kiasi cha sh 500,000 itatolewa bure.

MUHIMU: MWEKEZAJI AKATE KIAMBATANISHI KILICHOKO KWENYE FOMU YA MAOMBI NA KUBAKI NACHO KWA AJILI YA KUMBUKUMBU BINAFSI

====================